July 2024

# Zana za Viashiria vya Kila Mtoto Mchanga - Uboreshaji wa Upimaji kwa Watoto Wachanga na Watoto Waliozaliwa Wafu (EN-MINI) Zana za Mifumo ya Kawaida ya Taarifa za Afya


## Ew3 Zana za EN-MINI ni nini?

Zana za Viashiria vya Kila Mtoto Mchanga - Uboreshaji wa Upimaji kwa Watoto Wachanga na Watoto Waliozaliwa Wafu (EN-MINI) huongoza hatua za kipaumbele kwa ajili ya kuboresha upatikanaji, ubora, na matumizi ya viashiria vya watoto wachanga na waliozaliwa wafu katika mifumo ya kawaida ya taarifa za afya (MTUHA). Zana hizi zinapatikana bila malipo yoyote, ni rahisi kutumia, na hutoa ripoti zinazojizalisha kielektroniki kwa matumizi katika ngazi ya wilaya na kitaifa ili kusaidia Mpango wa Utekelezaji wa Kila Mtoto Mchanga (ENAP).

Zana za EN-MINI zimeundwa ili kuboresha taarifa zilizo kwenye mfumo wa taarifa za afya (MTUHA) ambazo zinaweza kutumika kupitia maendeleo na utendaji huku zikiwezesha matumizi ya data katika utungwaji wa sera na kuchukua hatua kwa ajili watoto wachanga na watoto waliozaliwa wafu. Zana hizi zinaimarisha mawasiliano kati ya wadau muhimu na kuwezesha kuwepo kwa taarifa sanifu kama inavyopendekezwa katika mwongozo wa kimataifa.

Zana za EN-MINI zinazingatia **kiashiria cha msingi cha watoto wachanga na watoto waliozaliwa wafu ni** kipimo kinacho oneshwa kama duru za taarifa za rangi ya chungwa katikati ya piramidi ya taarifa katika Kielelezo 1. Zana hizo saba zimewekwa katika makundi matatu- **Onesha namna taarifa za Watoto Wachanga zilivyopangiliwa, Tumia taarifa za Watoto Wachanga kwa ajili ya Kufanya Maamuzi** na **boresha Ubora wa kiwango cha taarifa za Watoto Wachanga**.

**Kielelezo cha 1.**
**Zana za EN-MINI na Piramidi ya Taarifa**




Adapted from: Day LT, Moran AC, Jackson D, et al. (2019). Survive and Thrive: Transforming care for every small and sick newborn. Chapter 5, Figure 5.1. Geneva, Switzerland.

## Zana za EN-MINI zilitengezwaje?

Toleo la 1 la zana za EN-MINI lilitengenezwa kama sehemu ya utafiti wa pili wa Ufuatiliaji wa Kiashiria cha Kila Mtoto Mchanga - hospitalini (EN-BIRTH)-2 , ulifikiriwa na kutekelezwa kwa kushirikiana na D4I; Kituo cha Kimataifa cha Maradhi ya Kuhara na Utafiti wa Magonjwa, Bangladesh (icddr,b); Taasisi ya Afya ya Ifakara (IHI); Chuo Kikuu cha Afya na Magonjwa ya Kitropiki cha London (LSHTM). EN-BIRTH 2 ilifadhiliwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia Data for Impact (D4I). Utafiti wa USAID kwa ajili ya Wafanya Waamuzi (RDM) kama sehemeu ya awali zilizofadhiliwa nchini Bangladesh, chini ya icddr,b. Utafiti wa Kuboresha Kiwango na Matumizi ya Viashiria Vya Mtoto Mchanga (IMPULSE) uliofadhiliwa na Chiesi Foundation ulichangia kuandikwa kwa toleo la 2.0 la Zana za EN-MINI.

Muhtasari huu unahusu *Viashiria vya Kila Mtoto Mchanga - Uboreshaji wa Upimaji wa Watoto Wachanga na Watoto Waliozaliwa Wafu (EN-MINI) Zana kwa ajili Mifumo ya Taarifa za Afya*, na The London School of Hygiene & Tropical Medicine UK, Taasisi ya Afya ya Ifakara Tanzania, icddr, b Bangladesh, na Data for Impact (2022).

# Ni nani anayeweza kutumia Zana za EN-MINI?

Zana za EN-MINI zilitengenezwa kwa ajili ya timu zinazofanya kazi ili kuboresha taarifa za watoto wachanga timu hizi uhusisha watunga sera na wasimamizi wa huduma za watoto wachanga ngazi ya wilaya na kitaifa, wadau wanaohusika na programu za watoto wachanga, na wataalamu wa mifumo ya taarifa za afya. Zana saba za EN-MINI zinaweza kutumika kwa pamoja lakini pia zinaweza kutumika kama zana moja moja. Zana za EN-MINI zinapatikana katika lugha nne- Amharic, Kiingereza, Kifaransa, na Kiswahili- kwa msaada wa USAID na Chiesi Foundation.


# Zana za EN-MINI zinahusisha nini?




## Kuonesha namna Taarifa za Watoto Wachanga zilivyopangiliwa

**Zana 0 ya kuonesha namna taarifa za watoto wachanga zilivyopangiliwa** imeundwa kupanga taarifa ya watoto wachanga katika viwango tofauti kwenye piramidi ya taarifa kutoka kwenye rejesta za kawaida za kituo cha tiba kwenye mfumo wa taarifa za afya (MTUHA) ya kielektroniki na ina matumizi matatu:

- Kupata taarifa za MTUHA za watoto wachanga na waliozaliwa wafu ambayo inaweza kutumika sasa kufuatilia maendeleo
- Kutambua mapungufu ya taarifa ya kawaida kwa kile unachohitaji na unachotaka kupima
- Kuchunguza ukubwa wa kazi, ikiwa ni pamoja na wahudumu wa afya




## Tumia Taarifa ya Watoto Wachanga kwa ajili ya Kufanya Maamuzi


Zana nne za EN-MINI zinashughulikia **Matumizi ya Taarifa za Watoto Wachanga.** Zana hizi zilitoholewa kutoka kwenye zana za Utendaji wa Mfumo wa Taarifa za Kawaida (PRISM) zilizotengenezwa na MEASURE EVALUATION. Zana hizi nne zina zana za kukusanya taarifa za kidigitali ambazo ziko tayari kutumika na kusaidia watumiaji:

- Kujifunza kuhusu ni taarifa zipi za ziada ambazo watumiaji wanahitaji kufuatilia maendeleo kwa watoto wachanga na watoto waliozaliwa wafu

**Zana ya 1 ya EN-MINI-PRISM** inachunguza vigezo vya kiufundi na kiwango cha mgawanyiko wa taarifa za MTUHA na upungufu ili kusaidia kuanzisha majadiliano ya ujumuishaji na matumizi ya taarifa.
**Zana ya 3 ya EN-MINI-PRISM** inachunguza utendaji na urahisi wa kutumia teknolojia inayotumika kuzalisha, kuchakata, kuchambua, na kutumia taarifa ya kawaida ya afya. **Zana ya EN-MINI-PRISM 4** inachukua rekodi za haraka za kanuni za usimamizi wa taarifa za MTUHA ili kusaidia maendeleo ya mipango ya utekelezaji na usimamizi ulioboreshwa. **Zana ya 6 ya EN-MINI-PRISM** inatambua na kubainisha vigezo vya kitabia na kimpangilio ambavyo vinaboresha utaratibu wa taarifa.

## Kuboresha ubora wa taarifa za Watoto Wachanga

Zana mbili za EN-MINI zinachangia katika kutathmini na KUBORESHA Ubora wa taarifa za Mtoto Wachanga. **Zana ya EN-MINI-PRISM 2** huamua kiwango cha jumla cha utendaji wa taarifa za MTUHA kulingana na ubora wa taarifa na matumizi ya taarifa. **Zana ya 5 ya EN-MINI-PRISM** inatathmini upatikanaji na hali ya rasilimali zinazohitajika kwa utekelezaji wa taarifa za MTUHA katika viwango vya usimamizi. Zana hizi mbili huwasaidia watumiaji: Kuangalia ubora wa taarifa ya watoto wachanga na waliozaliwa wafu




- Kuhakikisha kama njia za kutoa maoni zinafaa
- Kuchunguza zana zipi zinazohitajika ili kuboresha zaidi Kiwango cha taarifa

EN-MINI tools

## Kuboresha Afya za Watoto Wachanga Kupitia Utekelezaji wa Zana za EN-MINI nchini Tanzania

Utekelezaji wa Zana za EN-MINI nchini Tanzania ulikuwa mpango shirikishi na muhimu uliowahusisha watunga sera, wataalamu wa huduma za afya, na wataalamu wa mifumo ya taarifa za afya. Mpango huu unalenga kuboresha kiwango cha taarifa na matumizi katika ngazi tofauti ndani ya mfumo wa huduma za afya. Vilevile, mpango huu unawekea mkazo jukumu muhimu la wataalamu wa huduma ya afya katika kuboresha kiwango cha taarifa na unasisitiza kuhusu hali ya motisha ya kitamaduni kwa ajili ya viashiria vya watoto wachanga na watoto waliozaliwa wafu.

### Hatua Muhimu:

- **Mapendekezo katika Mpango wa Utendaji wa Mwaka 2022/2023:** Zana za EN-MINI zilipendekezwa kwa ajili ya kufuatilia viashiria vya watoto wachanga na waliozaliwa wafu kwenye mfumo wa kitaifa wa taarifa za usimamizi wa afya wakati wa uandaaji wa mpango wa utendaji wa kila mwaka wa afya ya uzazi, uzazi, watoto wachanga, watoto na vijana wa rika balehe (RMNCAH).
- **Kuwasilisha kwenye Mkutano wa kwanza wa Kimataifa wa Afya ya Uzazi na Watoto Wachanga (IMNHC) 2023:** Zana za EN-MINI zilitambulishwa kidunia katika IMNHC kwenye mkutano wa kwanza wa kimataifa wa afya ya uzazi na watoto wachanga 2023, na uliivutia timu ya mradi wa Laerdal Foundation's Safe Birth Bundle of Care (SBBC), ambayo iliahidi kuziingiza zana hizi kwenye programu yao.
- **Upanuzi wa Zana za EN-MINI nchini Tanzania na kwingineko:** Mafanikio ya kuingizwa kwa zana za EN-MINI katika mkoa wa Tanga ya lifungua njia ya utafiti wa Kuboresha Ubora na Matumizi ya Viashiria vya Watoto Wachanga. Katika Nchi za Kiafrika mradi wa IMPULSE, unazitumia zana hizi kutathmini viashiria vya watoto wachanga katika nchi nyingi, ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Afrika ya Kati, Ethiopia, Tanzania, na Uganda.

### Matokeo Yanayoweza Kutekelezwa kutoka kwa Utekelezaji wa Zana za EN-MINI nchini Tanzania:

- **Utendaji thabiti**: Maeneo yanayotambuliwa ya utendaji thabiti ni pamoja na matumizi madhubuti ya taarifa kwa ajili ya kufanya maamuzi na uboreshaji wa kiwango cha taarifa, hasa katika vigezo vya muundo na usahihi wa uingizaji wa taarifa katika ngazi ya wilaya.
- **Mapungufu yaliyobainishwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi**: Maeneo yaliyobainishwa kwa ajili ya uboreshaji ni pamoja na kuimarisha utamaduni wa matumizi ya taarifa/ taarifa kwenye vituo vya tiba, kuimarisha uchambuzi na kuwasilisha taarifa za watoto wachanga, na kuboresha motisha na weledi wa wafanyakazi wanaotoa huduma za afya.

### Mapendekezo:

- **Ujumuishaji wa kimkakati:** Zana za EN-MINI zinapaswa kuingizwa katika ziara za usimamizi wa utoaji wa huduma za afya z kawaida za ufuatiliaji ili kuwezesha tathmini ya kimfumo na uboreshaji endelevu wa ubora katika viwango vya vyote vya uto huduma ya afya.
- **Kuimarisha uwezo**: Kutoa kipaumbele kwenye mafunzo na msaada kwa wafanyakazi wa kituo cha tiba wanaohudumia j kuongeza weledi na motisha kwenye matumizi ya taarifa za MTUHA.
- **Kuboresha michakato:** Kurahisisha michakato ya taarifa za MTUHA ili kupunguza mzigo wa taarifa, thibitisha ukamilifu w taarifa, na hakikisha uwasilishaji wa taarifa kwa wakati.
- **Kusaidia kuhimiza matumizi ya taarifa:** Kuwezesha matumizi ya taarifa kwa ajili ya huduma za watoto wachanga, ubor wa ubora, na kufanya maamuzi ya kimkakati katika ngazi za wilaya na vituo vya tiba.

Utekelezaji wa matumizi ya zana za EN-MINI nchini Tanzania unaweza kuchochea maboresho makubwa katika matokeo ya afya ya watoto wachanga na watoto waliozaliwa wafu kwa kuboresha kiwango cha taarifa, matumizi ya taarifa, na kufanya maamuzi ya kimkakati katika mfumo wa huduma za afya. Ushirikiano unaoendelea na vitendo mahusus ni muhimu katika kuendeleza na kupanua athari hizi chanya.

**Ili kupata maelezo zaidi kuhusu nyenzo za EN-MINI, tafadhali tembelea**
www.data4impactproject.org/resources/en-mini-tools

Chapisho hili lilitolewa kwa msaada wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) chini ya masharti ya Data for Impact (D4I) mshirika nambari 7200AA18LA00008. Maoni yaliyotolewa hapa si ya maoni ya Serikali ya Marekani au USAID. FS-24-659a D4I

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE · DATA FOR impact · LONDON SCHOOL of HYGIENE &TROPICAL MEDICINE · MARCH MATERNAL ADOLESCENT REPRODUCTIVE & CHILD HEALTH · ISO 9001: 2015 certified IFAKARA HEALTH INSTITUTE research | training | services · MUHAS · icddr,b